MPANGO WA TASAF III.

KITENGO CHA TASAF

UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ni miongoni mwa Wilaya 16 zinazojumuisha Wilaya 14 za Tanzania Bara na Mamlaka za utekelezaji 2 kwa upande wa Zanzibar. Kundi hili ni maarufu kwa jina la **IMPACT WAVE** 5 au **SPECIAL WAVE 5** ambalo linahusika na zoezi maalum la upimaji/tathimini ya matokeo (yaliyotegemewa na yasiyotegemewa) ya utekelezaji wa mpango wa TASAF awamu ya tatu Lengo likiwa;

(i) Kuangalia na kupima kama mpango umefikia malengo yaliyokusudiwa.

(ii) Kuangalia kama muundo wa mpango katika hatua mbalimbali unaweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Katika kufanikisha zoezi hilo la upimaji wa matokeo ya utekelezaji wa mpango kwa Halmashauri za wimbi maalum 5 ni tofauti na Halmashauri nyingine kwa mambo yafuatayo;

(i) Vijiji vitapata Ruzuku peke yake(**Cash transfer only)**

(ii) Vijiji ambavyo vitapata ruzuku na miradi ya miundombinu **(Money transfer+Public works project).**

(iii) Vijiji ambavyo havitapata huduma yeyote kwa kipindi cha miezi 18

(**Control)** na baada ya zoezi la utafiti vijiji hivyo vitaingia katika utaratibu wa malipo ya ruzuku kwa walengwa wa mpango.Lifuatalo ni jedwali kuonyesha mgawanyo wa vijiji 14 kwa kundi la utafiti

Jedwali Na.1; Vijiji 14 Vya Kundi La Ki-Utafiti

i.	Vijiji ambavyo vitapata ruzuku pekeyake (Cash transfer only) **Kashinga,Rulenge,Shanga,Mukididili na Kumtana.**	5
ii.	Vijiji ambavyo vitapata ruzuku na miradi ya miundombinu (Cash transfer + Public Works Project)**Muruvyagira,Ntobeye,Kasulo,Mwivuza na Kumuzuza.**	5
iii.	Vijiji ambavyo havitapata huduma yoyote kwa kipindi maalum cha miezi 18(Control)na baada ya utafiti vitaendelea na taratibu za malipo.**Nyarulama,Mumiramira,Kihinga na Kumwendo**.	4

Aidha vijiji 42 vilivyobaki ambavyo havipo katika makundi matatu hapo juu vitaendelea na zoezi la malipo ya ruzuku kama ilivyopangwa.

Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ina jumla ya vijiji 56 vilivyopo kwenye mpango wa TASAF awamu ya III. Vijiji 42 vinapata ruzuku ya malipo kwa walengwa na vijiji 14 vipo katika kundi la utafiti. Aidha vijiji 42 ambavyo havikujumuishwa kwenye kundi la utafiti vinapata malipo ya ruzuku ya msingi na ya masharti.

Halmashauri ya wilaya ya Ngara ilianza na jumla ya kaya 8002 ambazo ziliandikishwa kutoka katika vijiji 52 vinavyotekeleza mpango wa kunusuru kaya maskini wa TASAF III.Hadi kufikia mwezi Julai 2018 Halmashauri inahudumia jumla ya kaya za walengwa 7748, kaya hizi zimepungua kutokana na vifo,kuhama makazi n.k.

2.0 MAPOKEZI YA FEDHA NA MATUMIZI YAKE

Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kwa mwaka wa fedha 2017/18 ilipokea kiasi cha Tsh. 2,263,614,160.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Uhawilishaji wa fedha,malipo ya ujira kwa kazi za muda kwa walengwa na uimarishaji wa uchumi wa kaya na kuweka akiba ambapo hadi kufikia Juni 2018 kiasi cha Tsh2,259,658,160.00 zilitumika na Tsh. 3,956,000.00 zimerudishwa Tasaf Makao Makuu na kufanya jumla ya matumizi kuwa Tsh. 2,067,881,300.00 na kubakiza salio la Tsh 186,852,860.00 utekelezaji wake unaendelea kwa mwaka wa fedha 2018/19 ambazo ni za kukamilisha shughuli za utekelezaji wa miradi ya kutoa ajira za muda kwa walengwa wa Tasaf III

.Aidha katika kipindi cha Robo ya kwanza kwa mwaka wa fdha 2018/2019 jumla ya Tshs.650,722,300.00 zimepokelewa kwa ajili ya malipo ya ruzuku naUjira kwa kaya za Walengwa wa Mpango wa kunusuru kaya masikini wa TASAF III.

Katika kipindi cha dirisha la Julai-Agosti 2018 kiasi cha Tshs. 635,961,800.00 zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa zoezi la uhawilishaji fedha kwa kaya za Walengwa 7,748 na malipo ya Ujira kwa kaya 6485 za Walengwa wa Kaya Masikini wa TASAF III.

waliofanyakazi za ajira muda (PWP) kipindi cha Februari na Machi 2018.Fedha hizi zimepokelewa kwa mgawanyo ufuatao ambapo Tshs. 266,060,000.00 ni kwa ajili ya malipo ya ruzuku kwa Walengwa,Tshs. 364,701,800.00 ni kwa ajili ya malipoya Ujira kwa Walengwa waliofanyakazi na Tshs 19,960,500.00 .ni kwa ajili ya gharama za Usimamizi.Adha zoezilamalipo ya fedha hizo yanatajiwa kuanza tarehe 07/08/2018 na kukamilika tarehe 15/08/2018.

Mapokezi ya fedha katika Zoezi la malipo ya Ruzuku Julai 2017 –Juni 2018

Na	Kipindi cha malipo	Fedha zilizopokelewa	Matumizi	Salio
1	Julai – Augosti 2017	253,912,000.00	252,712,000.00	1,200,000.00
2	Septemba – Octoba 2017	252,416,000.00	251,712,000.00	704,000.00
3	Novemba – Desemba 2017	252,584,000.00	251,872,000.00	712,000.00
4	Januari – Februari 2018	253,796,000.00	253,224,000.00	572,000.00
5	Machi- Aprili 2018	253,428,000.00	253,216,000.00	212,000.00
6	Mei- Juni 2018	253,912,000.00	253,632,000.00	280,000.00
7	**Jumla**	**1,520,048,000.00**	**1,516,368,000.00**	**3,680,000.00**

Mapokezi ya fedha katika Zoezi la malipo ya Julai –Agosti 2018/2019

Na	Kipindi cha Malipo	Fedha zilizopokelewa	Matumizi	Salio
	Julai- Agosti 2018	266,060,000.00	0	266,060,000.00

NB:Malipo haya yanatarajia kuanza tarehe 07/08 hadi 15/08/2018

Mapato na Matumizi ya Utekelezaji wa Miradi ya Kutoa Ajira za Muda (PWP)

Na	Shughuli	zilizopokelewa	Matumizi	Salio
i.	Zoezi la uibuaji wa miradi(PWP)	27,073,900	27,073,900	0.00
ii.	Zoezi la mafunzo kwa wasimamizi wa miradi ya kutoa ajira za muda(PWP)	26,312,800.00	26,312,800.00	0.00
iii	Gharama za usimamizi wa miradi 73,ununuzi wa vifaa pamoja na ujira wa LSP na CMC.	208,496,860.00	110,297,436.70	98,199,423.30
iv	Malipo kwa walengwa wa mpango wa TASAF III waliofanya kazi za ujira wa muda kwa vipindi Desemba 2017.	216,331,100.00	216,262,100.00	69,000.00
vi	Malipo kwa walengwa wa mpango wa TASAF III waliofanya kazi za ujira wa muda kwa vipindi Januari 2018.	236,451,500.00	236,244,500.00	207,000.00
vii	Malipo kwa walengwa wa mpango wa TASAF III waliofanya kazi za ujira wa muda kwa vipindi Februari na Machi 2018 dirisha la Julai-Agosti 2018	364,701,800.00	0	364,701,800.00
	Jumla	**1,079,367,960.00**	**616,190,737**	**463,177,223.30**

Jedwali na.2.4. Mapato na Matumizi ya Utekelezaji wa Mpango wa Kuweka Akiba kwa Walengwa wa TASAF III.

Na	Shughuli	Fedha zilizopokelewa	Matumizi	Salio
i.	Gharama za mafunzo kwa wawezeshaji wa uundaji wa vikundi vya Akiba.	17,635,000.00	16,745,000.00	890,000.00
ii.	Gharama za mafunzo kwa Madiwani,Wakuu wa idara na vitengo juu ya uundaji wa vikundi vya kuweka Akiba.	11,265,000.00	11,265,000.00	0
	Jumla	**28,900,000.00**	**28,010,000.00**	**890,000.00**

3.0 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MPANGO

Katika kipindi cha Mwaka 2017/18 Halmashauri ya Wilaya ya ngara inaendelea kutekeleza miradi mitatu ya Mpango wa Tasaf III wa kunusuru kaya Masikini ambayo ni:

1. Mradi wa Uhawilishaji wa Fedha kwa kaya Masikini(CCT)
2. Mradi wa Kutoa ajira za Muda kwa walengwa wa Mpango wa TASAF III (PWP).
3. Mradi wa kuhamasisha walengwa kuimarisha uchumi wa kaya na kuunda vikundi vya kuweka akiba (LE).

4.0. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KUTOA AJIRA ZA MUDA KWA WALENGWA WA MPANGO WA TASAF.

Halmashauri ya Wiaya ya Ngara ina jumla ya vijiji 52 vilivyopo kwenye Mpango kati ya vijiji hivyo ni vijiji 47 vinatekeleza miradi ya kutoa ajira za muda kwa kaya masikini. Zoezi la uibuaji wa miradi hiyo ya ya kutoa aijra za muda lilianza tarehe 10/10/2017 na kukamilika tarehe 20/10/2017 na jumla ya miradi 73 iliibuliwa na kupitishwa na Tasaf Makao Makuu kwa ajili ya utekelezaji kama ifuatavyo:-

- Miradi ya upandaji miti 34
- Miradi ya ujenzi wa vyanzo vya maji 15
- Miradi ya ujenzi wa marambo ya mifugo 4
- Utengenezaji wa Barabara 1
- Miradi ya kilimo 19

Miradi hiyo inatarajia kutumia kiasi cha shilingi Bilioni moja,milioni mia mbili na nne ,laki sita tisini na tano elfu mia saba ishirini tu(1,204,695,720/=ambapo jumla ya Tsh 452,782,600.00 zimetumika kulipa walengwa waliofanya kazi za ujira wa muda kwa kipindi cha Desemba 2017 na Januari 2018.Aidha Halmashauri ya wilaya Ngara imepokea kiasi cha Tsh 208,496,860.00 kwa ajili ya gharama za usimamizi na uendeshaji,ununuzi wa vifaa na vitendea kazi,ujira wa CMC na wasimamizi wa miradi(LSP).

Pia Halmashauri ya wilaya Ngara kwa mwaka wa fedha 2018/19 imepokea kiasi cha Tshs.364,701,800.00 kwa ajili ya malipo ya ujira wa muda kwa walengwa 6485 waliofanya kazi kipindi cha Februari na Machi 2018 na malipo yataanza tarehe 07/08/2018 na kukamilika tarehe 15/08/2018.

5.0 UTEKELEZAJI WA MRADI WA UHAMASISHAJI WA WALENGWA KUIMARISHA UCHUMI WA KAYA NA KUUNDA VIKUNDI VYA KUWEKA AKIBA.(LE)

Mafunzo kwa wadau wa utekelezaji wa mpango wa kuhamasisha walengwa kuimarisha uchumi wa kaya na kuunda vikundi vya kuweka akiba kwa walengwa wa mpango wa TASAF III yametolewa kwa makundi yafuatayo:-

Jedwali 2.5 Kuonyesha Idadi Ya Washiriki Na Jinsia.

Na	Washiriki	Idadi ya washiriki		
		ME	**KE**	**JUMLA**
1	Wakufunzi(TOT)	12	8	**20**
2	Kamati ya Wataalam (CMT)	29	4	**33**
3	Waheshimiwa Madiwani	25	6	**31**
4	Maafisa ugani ngazi ya Kata(WAEO)	7	13	**20**
JUMLA		**73**	**31**	**104**

Baada ya mafunzo jumla ya vikundi 33 viliundwa katika vijiji 4 ambapo Buhororo vikundi 8,Murugarama vikundi 8,Munjebwe vikundi 8 na Magamba vikundi 9.
Aidha uundaji wa vikundi kwa vijiji 43 utaendelea katika awamu ya pili ya uwezeshaji sambamba na kupewa ruzuku toka Tasaf Makao Makuu ili kuendeleza vikundi hivyo.

6.0 CHANGAMOTO:-

Pamoja na mafanikio kumekuwa na changamoto zifuatazo:-

- Pamoja na kupata muongozo mpya wa malipo kutoka TASAF Makao Makuu kwa Wasimamizi wa mradi ngazi ya Jamii CMC wameendelea kulalamikia kiwango cha malipo ya Tsh, 10,000 kwa siku kwamba hakitoshi, na baadhi yao kujiuzulu kazi hiyo.
- Baadhi ya walengwa wa mpango kutotumia fedha wanazopokea kwa kila dirisha kwa malengo yaliyokusudiwa na mpango.(mfano,walengwa kutumia fedha za mpango kunywea pombe).
- Ucheleweshwaji wa malipo kwa wazabuni waliotoa huduma ya vifaa na vitendea kazi vya miradi ya PWP hivyo kuathili ukamilishaji wa utekelezaji wa miradi kwa wakati.
- Fomu za masharti ya elimu na afya zinazotumwa toka TASAF makao makuu huja zikiwa pungufu.mfano vijiji vya Muhweza na Mukaliza.
- Ukosefu usafiri wa uhakika kuathili shughuli za ufatiliaji wa miradi vijijini kwa wakati.
- Wataalam wachache (Technical expert) ukilinganisha na wingi wa miradi iliyoibuliwa katika sekta mbalimbali,(maji,,miti,ujenzi n.k.).

6.1 UFUMBUZI WA CHANGAMOTO

- CMC wameendelea kuelimishwa juu ya dhana ya kujitolea katika kusaidia kaya masikini.
- Elimu kwa walengwa inaendelea kutolewa kwa walengwa juu ya matumizi sahihi ya fedha wanazopokea kutoka kwenye mpango nakukumbushwa ya kuwa Ulengwa wao wa kuhudumiwa na TASAFni wa kipindi maalum muda ukifika utakoma .
- Idara ya fedha, Kitengo cha ugavi na Tasaf wanaendelea kushughulikia changamoto malipo kwa Wazabuni ili kuhakikisha wazabuni waliobaki wanalipwa fedha zao.